

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU

SHULE YA SEKONDARI NYANGUGE,
MAGU.

18/12/2021.

Kumb. Na. NYSS/VOL.1/3/13/2021

MZAZI/MLEZIWA _____

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYANGUGE
KIDATO CHA KWANZA 2021**

Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Nyanguge. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021, unatakiwa kumpatia mwanao mahitaji ya shule mapema iwezekanavyo ili asichelewe kufika shuleni siku ya kufungua.

Tutaanza na kozi ya kiingereza kwa muda wa wiki (8) kuanzia tarehe ya kufungua.

Ni muhimu mwanao ashiriki kozi hii kwani inamsaidia mwanafunzi kumudu masomo ya sekondari ambayo mengi yanafundishwa kwa kiingereza.

Soma kwa makini mahitaji unayotakiwa kumuandalia mwanao kabla hujamleta shuleni.

MAHITAJI:-

A. VIFAA

- i. Daftari 12 (tunashauri umnunulie **COUNTER BOOK QUIRE 2 AU QUIRE 3**)
- ii. Begi la kubebea daftari
- iii. Kalamu, rula, pensel, Mathematical set na Dictionary (English to English)
- iv. Fagio aina ya chelewa kwa ajili ya usafi.

B. SARE

a) WASICHANA

- ❖ Sketi 2 (rangi ya light blue) zenye marinda (2 ½ inch) ya kupanga, ziwe ndefu zinazogusa kisigino (jora suti grade One)
- ❖ Shati (02) nyeupe mikono mifupi
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba, visiwe na kisigino kirefu.
- ❖ Soksi nyeupe jozi mbili (02)
- ❖ Wanafunzi wa kike wa KIISLAMU washone sketi ndefu zenye marinda (2 ½ inch)zinazogusa kisigino na sio suruali.
- ❖ Hijabu ifuate utaratibu wa Hijabu inavyotakiwa kuwa (Kwa wanafunzi wa kiislamu wa kike)

- ❖ Rangi ya hijabu ifanane na rangi ya sare ya shule
- ❖ Sweta ya rangi ya kijivu
- ❖ Picha 4 passport size za rangi

b) WAVULANA

- ❖ Suruali (02) rangi ya light blue. Mshono wa kawaida (usio na madoido), mifuko mitatu, miwili mbele na mmoja nyuma, iwe na marinda mawili mbele, isiwe ya kubana yaani isiwe modo (Jora la Suti grade 1)
- ❖ Shati mbili (02) nyeupe mikono mifupi
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi visiwe na kisigino kirefu, vyenye kamba.
- ❖ Soksi nyeupe jozi mbili (02)
- ❖ Sweta rangi ya kijivu
- ❖ Picha 4 passport size za rangi

c) KWA WOTE SARE ZA MICHEZO:

- ❖ Raba
- ❖ Bukta na Tisheti rangi ya Blue (kwa wavulana)
- ❖ Truck suti na Tisheti rangi ya Blue (kwa wasichana)

d). CHAKULA .


Kwa kuzingatia Afya mwanao na makubaliano ya wazazi ya kuwapatia chakula cha mchana wanafunzi wote wawapo shuleni, Unashauriwa kumtolea mchango wa chakula mwanao ili aweze kusoma kwa utulivu awapo shuleni kwa mchanganuo ufuatao.

Muhula wa kwanza(Januaari-June)		Muhula wa pili(Julai - Desemba)	
Mchele	24kg	Mchele	24kg
Maharage	7kg	Maharage	7kg
Mpishi na mahitaji mengine.	7,000/=	Mpishi na mahitaji mengine.	7,000/=

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

- ❖ Iwapo mwanao hatari pota ndani ya wiki moja tangu shule ifunguliwe hatua kali zitachukuliwa dhidi yako mzazi/mlezi.
- ❖ Azisome sheria za shule na kuzielewa na awe tayari kuzifuata
- ❖ Atimize mahitaji yake kwa muda muafaka
- ❖ Mpeleke mwanao hospitali akapimwe na daktari nakujaziwa fomu ya uchunguzi wa afya kisha uilete shuleni siku ya kuripoti.

Nakutakia maandalizi mema


AYOUB . J LEO
MKUU WA SHULE

075503572

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NYANGUGE
MAGII

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI NYANGUGE

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE KWA MWANAFUNZI

A. HESHIMA/NIDHAMU

- i. Ni lazima kusimama na kumsalimia Mwalimu, Mfanyakazi au mtu yeyote. Anayekuzidi umri, anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
- ii. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya kwa wanafunzi wenzake, kwa walimu na kwa watu wengine akiwa ndani au nje ya eneo la shule.
- iii. Ni muhimu kwa mwanafunzi kuwaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni au nje ya shule kama walezi wake.
- iv. Wanafunzi wanatakiwa kushirikiana na kusaidiana katika kazi.
- v. Wanafunzi ni lazima kuitika na kukimbia aliko mkuu anayemuita.
- vi. Wanafunzi ni lazima waheshimu Bendera ya Chama na Serikali, picha za viongozi wa Chama na serikali, Nembo ya Taifa (Coat of Arms), Wimbo wa Taifa ama Fedha za Taifa.
- vii. Wanafunzi lazima waheshimu ukumbi wa mikutano, mahala pa kulia chakula, ofisi za shule, mali binafsi na mali ya Umma.
- viii. Daima wanafunzi watasimama katika mstari wakati wa kupata huduma.
- ix. Wanafunzi lazima waye mfano kwa heshima na tabia njema mahali popote walipo.
- x. Wanafunzi lazima wakae kimya wakati wote wanapo kuwa darasani, wasitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyemo darasani.
- xi. Wanafunzi lazima wasafishe na kuyatunza mazingira ya shule.
- xii. Ni marufuku kwa mwanafunzi:
 - a) Kuvuta sigara au kunywa vileo vya aina zote.
 - b) Kuvaa mavazi yasio ya shule awapo shuleni
 - c) Kugombana/kugombanisha akiwa ndani au nje ya mazingira ya shule
 - d) Kugoma/ kugomesha akiwa ndani au nje ya shule
 - e) Kuzomea/kutukana wenzake, walimu au watu wengine.
 - f) Kubaka akiwa ndani au nje ya shule
 - g) Kufanya uasherati/mapenzi ndani au nje ya shule.
 - h) Kuoja/kuolewa au kuweka/kuwekwa kimada.
 - i) Kupata au kutoa mimba, pia kusababisha mimba.
 - j) Kuficha ukweli/ ushahidi.
 - k) Kuibakitu cha mwenzake, cha shule au cha Umma
 - l) Kufanya magendo au biashara ndani au nje ya eneo la shule.
 - m) Kukaribisha wageni bila ruhusa
 - n) Kuharibu kwa makusudi kitu chake, cha mwenzake ama cha Umma.

- o) Kutoonesha ukarimu, kutopokea mizigo na kujituma kusaidia shughuli mbalimbali zinazokubalika
- p) Kutozingatia ratiba ya shule, kutoroka vipindi na mitihani darasani.

B. MAHUDHURIO

- i) Ni muhimu na lazima kuhudhuria shule kwa muda wote wa masomo.
- ii) Ni lazima mwanafunzi ahudhurie vipindi vyote vya ndani na nje ya darasa
- iii) Ni lazima mwanafunzi ahudhurie katika kazi za mikono.
- iv) Ni lazima wanafunzi wote wahudhurie mikutano ya shule kama vile Baraza la shule, ukaguzi wa mwili na mazingira, school parade, kupandisha Bendera ya Taifa, mikutano ya darasa, ukumbi wa chakula, vilabu (vyama) vya masomo, madhehebu ya dini (kiroho) kwa wenye imani hizi n.k.

C. KUWAHI (PANCTUALITY):

- i) Wanafunzi lazima wa thamini muda.
- ii) Wanafunzi lazima kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika utaratibu wa kila siku wa shule (School Daily Routine).
- iii) Ni lazima wanafunzi kuwahi popote wanaposikia wito wa dharura.
- iv) Ni lazima wanafunzi wafike shuleni kutoka nyumbani/likizo kwa tarehe zilizopangwa.
- v) Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni saa 12:45 asubuhi (Kuhesabu namba)

D. SARE ZA SHULE (SCHOOL UNIFORMS):

- i) Ni lazima mwanafunzi avae sare wakati wote wa:
 - a) Masomo darasani.
 - b) Kutoka nje ya shule kwa ruhusa na shughuli za kishule.
 - c) Baraza la shule.
 - d) Kusafiri kuja shuleni/ kwenda nyumbani wakati wa shule au likizo.
- ii) Ni lazimawanafunzikuwanavazi la kazi/michezo.
- iii) Kofia, ndala, viatu vya visigino virefu na mapambo mengine kama vile hereni, bangili, rangi za kucha lipsticks, powder, manukato ya harufu kali (cosmetics) na mitindo ya kusuka nywele (rasta, mabutu n.k hairuhusiwi shuleni) – labda kwa kibali maalum.

E. MIPAKA YA SHULE:

- i) Wanafunzi watatoka nje ya mipaka ya shule kwa kibali maalum kutoka kwa mkuu wa shule.
- ii) Wanafunzi hawaruhusiwi kutembea sehemu zifuatazo:-
 - a) Vilabu vya pombe (Bar).
 - b) Majumba ya kufikia wageni (Guest House)
 - c) Majumba ya starehe (Disco, Dansi, Video n.k)

F. USAFI:

- Usafi ni sehemu muhimu ya maisha ya mwanafunzi hivyo:-
- a) Ni makosa kwa mwanafunzi kuvaa sare chafu.

- b) Wanafunzi wafuate kanuni za usafi wakati wote wanapokuwa shuleni na nje ya shule.
- c) Wanafunzi watapaswa kuwa na nywele fupi zinazoweza kuchanwa kwa kitana, sio kunyoa kwa mitindo kama vile kiduku, panki, kipara n.k.
- d) Wanafunzi wasichafue mazingira kwa :-
 - Kujisaidia hovyoy, kutupa taka hovyoy, kukatisha viwanja na kukata au kuvunja miti / maua ya shule.
- e) Ni marufuku kufuga ndevu au kucha.

G. KUJITUMA UBORA NA BIDII YA KAZI

- 1. Lazima kila mwanafunzi afanye kazi kwa bidii na ubora wa hali ya juu.
- 2. Kila mwanafunzi anapaswa kusoma kwa bidii, **kamwe uvivu haukubaliki.**

H. MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

- 1. Wizi
- 2. Uasherati
- 3. Ulevi wa aina yoyote
- 4. Uvutaji wa bangi/madawa ya kulevya
- 5. Makosa ya jinai
- 6. Kuharibu kwa makusudi mali za umma
- 7. Kupiga /kupigana
- 8. Kudharau bendera ya Taifa
- 9. Kupata/kutoa/kuolewa au kusababisha mimba
- 10. Mgomo /kuongoza mgomo/kuchochea mgomo/kuvuruga amani na usalama wa shuleni au watu
- 11. Kubaka, kuweka au kuwekwa kimada
- 12. Kunyanyasa wanafunzi wengine
- 13. Utoro wa kudumu (siku 60 mfululizo au 90 rejareja)
- 14. Kukataa adhabu kwa makusudi
- 15. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni

(Signature)

**AYOUB J.LEO
MKUU WA SHULE**

**MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NYANGUGU
MAGI**

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIONS
NYANGUGE SECONDARY SCHOOL

PART A:- Full Name _____
Age _____ Height (cm) _____ Weight _____

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for joining secondary school. The examination should include the following categories. (I -III) each category of sub category of which, will render the applicant ineligible in each of a defect. Pregnancy (Plan test) category IV will also render a girl student ineligible.

- I. (a) Eye sight _____
(b) Hearing _____
(c) Speech _____
(d) Venereal disease (HIV) _____
(e) Leprosy and T.B disease _____
(g) Spleen _____
(h) Chest /Abdomen _____
(i) Blood count _____
(j) Urinalysis _____
- II. Neuroses _____
- III. Additional indermation eg. Physical defects or impairments
Infections chronic or family /heritable disease (=Sickle cell) inability to eat certain food at _____
- IV. Pregnancy _____

PART B:

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government medical officer)

I have examined the above named school student and consider that she/he is physically and mentally fit/unfit to join full time Secondary Education Course.

Name and Signature _____

Designation _____

Station _____

Date _____

TAMKO LA MWANAFUNZI (Ijazwe na irudishwe shuleni)

Mimi (jina) _____ ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza shule ya sekondari Nyanguge. Nimesoma na kuzielewa sheria na kanuni za shule. Hivyo nakubaliana/sikubaliani na sheria na kanuni zote za shule. Naahidi kuzifuatana kuzitii zote kama zilivyoelekeza.

Sahihi ya mwanafunzi _____

Tarehe _____

MAONI YA MZAZI / MLEZI (Yaruddishwe shuleni)

Mimi (jina) _____ Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi (jina) _____ nimesoma sheria na kanuni za shule, nimemshirikisha mwanangu na nimezielewa vizuri. Hivyo nakubaliana/ sikubaliani na sheria hizi na kanuni za shule.

Nimeamua mwanangu asome/asisome shuleni hapo.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi _____

Namba ya simu _____

Tarehe _____